

*Shairi, Utenzi huu uliandikwa na Christopher Chacha Mwita, katika lumbano la kishairi na Hassan Adam wa Cologne, Ujerumani.*

1. Uliyoyasema muruwa, dunia imebadilika.  
Enzi tukiaswa, wanyumbani akubalika.  
Lakini tukagunduwa, msukuma anaoleka.  
Mdengereko chukuwa, muhimu anaoleka.
2. Zama za nyuma huko, wakabila asifiwa.  
Ati ana miiko, itakiwayo na wakubwa.  
Wengineo miiko, wanaivuwa kwa wakubwa.  
Lakini mabadiliko, yametufunza muruwa.
3. Jamaa walijaribu, kumbe warangi wafaa.  
Pia katika majaribu, wakakuta wasukuma muruwaa.  
Baadaye wakastaajabu, kwa yale yaliyowajaa.  
Kumbe wale wakabila, sawa na wengine kufaa.
4. Zama za wa kwetu kufaa, sasa hazina nafasi.  
Muhimu ni wewe kukaa, kupima uliyonayo nafasi.  
Ukikuta yanafaa, na unaweza kuyapa nafasi.  
Basi oa anayekufaa, ya kwake pia uyape nafasi.
5. Beti tano tamati, hii si fani yangu.  
Mmasai, mmanga'ati, oa ndugu yangu.  
Mdachi au mgiriki, upendo ndugu yangu.  
Kama upendo umediriki, kitaondoleka kiwingu.

*Christopher Chacha Mwita, (CCM)  
Alabama, USA  
mshairi mwanafunzi  
Julai, 2002*